

Matini iliyosomwa na Soi mbele ya wanafunzi iliwafaa wenzake sana. Wote waliketi kwa utulivu huku wakisikiliza kwa makini habari iliyowasilishwa kwenye matini hiyo. Ujumbe uliowasilishwa ulihusu athari za shinikizorika kwa vijana. Athari zenyewe zilikuwa nyingi. Hata hivyo, iliyosisitizwa sana ni kwamba shinikizorika linaweza kumfanya mtu kupotoka kimaadili. Wanafunzi walifurahia kupata habari hizo kwa sababu ziliwasaidia kukabiliana na shinikizorika.